

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Anwani ya Simu: "TUME"

DODOMA

Nambari ya Simu: 0738 166 703

0733 005 974

Barua pepe: secretary@psc.go.tz

Tovuti: www.psc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Umma,
Jengo la Chimwaga (UDOM),
Ghorofa ya 2,
2 Barabara ya UDOM,
S.L.P. 1074,
40405 DODOMA.

TANGAZO

NAFASI ZA UHAMISHO KWA WATUMISHI WA UMMA

Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma (OR-TUU) imeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 9 (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 (Marejeo ya Mwaka 2019) ikiwa na majukumu ya kusimamia na kuhakikisha usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma unafanyika kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zinazoongoza Utumishi wa Umma.

Tume ya Utumishi wa Umma inawatangazia watumishi wa Umma kuwepo kwa nafasi wazi kumi na nne (14) za kuhamia katika Kada mbalimbali. Nafasi hizo zipo katika Idara na Vitengo mbalimbali katika Ofisi za Tume zilizopo Jijini Dodoma.

Waombaji wenye sifa stahiki kwa mujibu wa Nyaraka za Maendeleo ya Utumishi (Miundo ya Utumishi) kwa kada husika na wenye nia ya kufanya kazi Tume ya Utumishi wa Umma wanashauriwa kuomba. Nafasi zilizo wazi ni kama inavyoonekana katika Jedwali lifuatalo:-

NAFASI ZA KUJAZA KWA NJIA YA UHAMISHO TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Na.	CHEO/KADA	IDADI YA NAFASI
1.	Afisa Utumishi Mwandamizi	6
2.	Afisa Utumishi Daraja la I	2
3.	Afisa TEHAMA Daraja la I	1
4.	Afisa Sheria Daraja la I	1
5.	Afisa Ukaguzi wa Ndani Daraja la I	1
6.	Afisa Ustawi wa Jamii Mwandamizi	1
7.	Mwandishi Mwendesha Ofisi Daraja la I	2
	JUMLA	14

Ili mwombaji aweze kufikiriwa kuhamia, anapaswa kukidhi vigezo vifuatavyo:-

1. Awe Mwajiriwa wa Serikali mwenye sifa stahiki kwa nafasi husika;
2. Barua ya maombi ipitishwe na Mwajiri na igongwe muhuri;
3. Aambatishe Vyeti vya Taaluma pamoja na matokeo (Transcripts);
4. Aambatishe Wasifu Binafsi (CV);
5. Aoneshe **Check Na./Namba ya Ajira** kwenye barua ya maombi; na
6. Athibitishe utayari wa kujigharamia uhamisho huo kwenye barua ya maombi.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **21 Juni, 2024.**

Maombi yote yaandikwe na kutumwa kwa:-

Katibu,
Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Umma,
Jengo la Chimwaga (UDOM),
Ghorofa ya Pili,
2 Barabara ya UDOM,
S.L.P. 1074,
40405 DODOMA.

Au

Barua pepe: secretary@psc.go.tz

Limetolewa tarehe 04 Juni, 2024.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Mathew M. Kirama', with a large circular flourish above the name.

Mathew M. Kirama

KATIBU

TUME YA UTUMISHI WA UMMA